# DHIBITI UGONJW WA UBWIRI UNGA WA MIKOROSHO KWA KUTUMIA KIUATILIFU CHA MAJI




*Kimetayarishwa na:*

TARI - Naliendele
Taasisi ya Utafiti wa Kilimo
S. L. P. 509
MTWARA - Tanzania
Email: cdnaliendele@tari.go.tz


**2026**

## 1.0 Utangulizi

Moja ya matatizo makubwa ya uzalishaji wa zao la korosho ni ugonjwa wa Ubwiri unga, ambao umeenea katika mikoa yote Tanzania. Ugonjwa huo husababishwa na vimelea aina ya kuvu na huweza kupunguza mavuno kwa zaidi ya asilimia 70.

## 2.0 Mashambulizi ya Ubwiri unga

- Hushambulia sehemu teketeke (majani, maua, mabibo na korosho changa) katika mkorosho.
- Husababisha maua kushindwa kufunguka kuchavushwa hatimaye kunyauka na kukauka.

## 3.0 Dalili za ugonjwa

Kuonekana kwa unga unga mweupe au/ na kijivu uliofunika sehemu teketeke za mkorosho.



*Dalili za Ubwiri unga kwenye majani*

- Majani yaliyoshambuliwa husinyaa, hubadilika rangj, wakati mwingine hukunjamana.
- Majani machanga zaidi yanaweza kupukutika.
- Majani machanga yaliyoshambuliwa yanapokomaa huwa na mabaka ya rangi ya kahawia
- Maua yaliyoshambuliwa sana hushindwa kuchanua na hatimaye hukauka kabisa na kuwa rangi ya kahawia



*Dalili za Ubwiri unga kwenye maua*

- Mabibo yaliyoshambuliwa hudumaa, huwa na mipasuko na hupoteza rangi yake.
- Korosho changa zilizoshambuliwa huweza kubadilika rangi na kupukutika.
- Korosho zilizoshambuliwa zikifikia kukomaa, hupoteza rangi ya kijivu na hutengwa katika daraja la pili.



Athari za Ubwiri unga kwenye bibo na tegu

## 4.0 Kuenea kwa ugonjwa

- Vimelea vya Ubwiri unga vinaishi kwenye mimea iliyo hai tu.
- Ugonjwa huu hustawi zaidi kuanzia mwezi may hadi septemba kipindi a mbacho mikorosho ina machipukizi mapya na inaanza kutoa maua.
- Ugonjwa pia hustawi zaidi kwenye jotoridi kati ya 26 hadi 28 sentigredi na unyevu hewani kati ya asilimia 80 hadi 100.
- Ubwiri unga hupendelea zaidi mikorosho iliyosongamana.
- Katika kipindi cha mwezi oktoba hadi April vimelea hujificha na kuishi kwenye maotea au machipukizi ambayo baadae huwa ni chanzo chaubwiri unga.

## 5.0 Kudhibiti Ubwiri Unga

Kuna njia tatu zinazotumika kudhibiti Ubwiri unga

### 5.1 Udhibiti sango

Kuondoa machipukizi na maotea ili kupunguza kasi ya kuenea ugonjwa wa Ubwiri Unga

- Kupogolea matawi ya mikorosho ili kuruhusu mzunguko wa hewa
- Ng'oa mikorosho iliyosongamana kwa kuzingatia uzaaji ili kuruhusu mzunguko wa hewa shambani.

### 5.2 Matumizi ya mbegu bora

- Panda mbegu bora zinazovumilia mashambulizi ya ugonjwa wa Ubwiri unga.

### 5.3 Matumizi ya Kiuatilifu cha maji

- Tumia kiuatilifu chenye kiambata kimojawapo kati ya hivi; Cypraconazole, Hexaconazole, dymethomorph + propamocarb hydrochloride.
- Changanya mililita 15 za kiuatilifu kwa lita moja ya maji.
- Puliza kiuatilifu kila baada ya siku 14-21 kutegemeana na mashambulizi.



## 6.0 KuchanganyaViuatilifu vya maji

Changanya viuatilifu vya maji kama ifuatavyo:-

i. Changanya kiuatilifu cha kudhibiti ugonjwa wa ubwiri unga na kiuatilifu cha wadudu waharibifu pale inapobidi.

ii. pulizia kila baada ya siku 14 - 21 kutokana na hali ya mashambulizi shambani